## 1.0.HISTORIA FUPI YA SHIRIKA LA MASISTA MITUME WA UPENDO UPEO (MMUU).

Mwaka 1985 Hayati Mhashamu Christopher Mwoleka, aliyekuwa Askofu wa Jimbo Katoliki la Rulenge wakati ule, alianzisha rasmi Shirika hili Oktoba 25, na 1987 kundi la kwanza la Masista watatu walifunga Nadhiri zao za Kwanza. Masista hao ni: 1. Sr. Mary Gurth 2. Sr. Veronica Hhari 3. Sr. Catharina Petro (alifariki tarehe 11/04/1991). Apumzike kwa Amani Mbinguni. Amina.

Mwaka 1996 Askofu Christopher Mwoleka alijiuzulu uongozi wa Jimbo la Rulenge wakati ule, kutokana na afya yake kuwa mbaya. Alifariki dunia Oktoba 16, 2002. Apumzike kwa Amani Mbinguni. Amina.

Novemba 8, 1996 Askofu Severine NiweMugizi aliteuliwa kuliongoza Jimbo la Rulenge wakati ule. Alilipokea Shirika la Masista Mitume wa Upendo Upeo na kulilea. Pia alitambua uhitaji wa Shirika hili kuendelea kulelewa zaidi, ili kuendana na taratibu na miongozo ya Sheria za Kanisa kwa Mashirika ya Kitawa.

Aliliomba na kuwakaribisha Shirika la Masista wa Mt. Theresia wa Mtoto Yesu kutoka Jimbo Katoliki la Bukoba, lisaidie kutoa Malezi kwa Shirika la Masista Mitume wa Upendo Upeo mpaka liweze kukua na kufikia hatua ya ukomavu unaostahili kujisimamia na kujiongoza. Agosti 14, 2008 Baba Mt. Benedikto wa 16 alitangaza kutengwa kwa Jimbo la Rulenge na kumteua Mhashamu Askofu Almachius-Vincent Rweyongeza kuwa Askofu wa Kwanza wa Jimbo Jipya la Kayanga. Sasa Shirika la Masista Mitume wa Upendo Upeo (MMUU) liko chini ya usimamizi wa Askofu Almachius-Vincent Rweyongeza.

### 1.1. WALEZI WA KWANZA WA MMUU

Malezi yaliyoongozwa na Shirika la Bathereza kipindi cha miaka kumi na mitano, yaani kuanzia 10/04/1999 hadi 25/11/2014. Walezi waliotulea kwa vipindi vitatu nyakati tofauti walikuwa ni tisa:-

1. Sr. Caritas Kokuteta
2. Sr. Floriana Kasano
3. Sr. Wilhelmina Kokugoshoka
4. Sr. Hyasinta Misingo
5. Sr. Sylivia Mkajaje
6. Sr. Rovina Francis
7. Sr. Florentina Ichaka
8. Sr. Godeliva Mboyerwa
9. Sr. Theophilda Irene.

### 1.2.MKUTANO MKUU WA KWANZA

Novemba 10, 2014 Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Shirika ulianza.

Novemba 25, 2014 Viongozi wa Kwanza wa Shirika la Masista Mitume wa Upendo Upeo (MMUU) wafuatao walichaguliwa:

1. Sr. Dafrosa C. Kabonesa Kiongozi Mkuu wa Shirika
2. Sr. Seraphina Stephano Makamu
3. Sr. Veronica Hhari Mshauri
4. Sr. Georgia Audax Mshauri
5. Sr. Florentina Pontian Mshauri

### 1.3.MKUTANO MKUU WA PILI

Septemba 21, 2019, Mkutano Mkuu wa Pili wa Shirika ulianza.
Oktoba 10, 2019, Viongozi wa Pili wa Shirika la Masista Mitume wa Upendo Upeo, Walichaguliwa kama ifuatavyo:

1. Sr. Dafrosa C. Kabonesa Kiongozi Mkuu wa Shirika.
2. Sr. Seraphina C. Stephano Makamu
3. Sr. Vestina N. Julius Mshauri
4. Sr. Veronica T. Hhari Mshauri
5. Sr. Adolphina W. Mwesiga Mshauri.

### 1.4.MAKAO MAKUU YA SHIRIKA NA MAKABURI.

Makao Makuu (Generalate) ya Shirika pamoja na makaburi ya wanashirika ya Shirika la Masista Mitume wa Upendo Upeo, yapo Bushangaro.

**IDADI YA WANASHIRIKA HADI SASA.**

Shirika la Masista Mitume wa Upendo Upeo, linaendelea kukua na kuzaa matunda.
hadi leo 24/09/2024:

| | |
|---|---|
| Jumla ya Masista ni | **108** |
| Nadhiri za Milele | 68 |
| Nadhiri za Muda | 40 |

**<u>KONVENTI ZA MASISTA</u>**

| | |
|---|---|
| Jimbo Katoliki la Kayanga | 14 |
| Jimbo Katoliki la Rulenge-Ngara | 01 |
| Jimbo Katoliki la Bunda | 01 |

**<u>ORODHA YA KONVENTI ZOTE:</u>**

1. Mt. Mathayo Bushangaro Nyumba Mama
2. Mt. Philomena Bushangaro

| | |
|---|---|
| 3. Mt. Cecilia | Bushangaro |
| 4. Malkia wa Amani | Bushangaro |
| 5. Moyo Mt. wa Yesu | Chabalisa –Bushangaro |
| 6. Mt. Ignas wa Loyola | Bugene |
| 7. Bikira Maria Msaada wa Daima | Uaskofuni Kasharara. |
| 8. Mt. Anthony wa Padua | Kimiza. |
| 9. Mt. Monica | Kaaro |
| 10. Mt. Yuda Thadei | Kitwe'Chenkula-Rukulaijo |
| 11. Mt. Augustini | Isingiro |
| 12. Mt. Theresia wa Mtoto Yesu | Businde |
| 13. Mt. Theresia wa Avila | Bugomora |
| 14. Mt. Theresa wa Kalkuta | Mabira |
| 15. Mt. Joseph – Rulenge | Ngara |
| 16. Mt. Maria Magdalena | Uaskofuni Bunda. |
| 17. Mt. Clara | Mwanza -Tarajiwa |
| 18. Mt. Agnes | Tabora –Tarajiwa |

**KONVENTI TARAJIWA**
Paroki ya Nyang'ngi Mwanza
Parokia ya Nyakatuntu
Jimbo Kuu la Tabora

**NYUMBA ZA MALEZI**
1. Kandegesho (Mt. Christopher) Mapostulanti na Manovisi
2. Isingiro (Mt. Yohana Paulo wa Pili) Maaspiranti na Makandidati.

**WANAFUNZI WA UTAWA**

| | | |
|---|---|---|
| Jumla ya wanafunzi wa Utawa | | **70** |
| Manovisi mwaka | II | 145 |
| Manovisi | I | 14 |
| Mapostulanti tarajiwa | | 15 |
| Maaspiranti | | 36 |

**1.5. KITUO CHA MALEZI YA MAASPIRANTI NA MAKANDIDATI.**
Kituo cha Malezi ya Awali Maaspiranti na makandidati yako Isingiro (Mt. Yohane Paulo wa Pili), Wilaya ya Kyerwa.

**1.5.1. KITUO CHA MALEZI YA MAPOSTULANTI NA MANOVISI.**

Kituo cha Malezi ya Mapostulanti na Manovisi yako Kandegesho (Mt. Christopher), Parokia ya Kayungu, Wilaya ya Karagwe.

### 1.6. TAASISI.

Tunayo taasisi moja ya Shule ya Awali na Msingi Mwoleka Mseto Chabalisa, Parokia ya Bushangaro.